TANGAZO LA SERIKALI Na.....324.....la tarehe.....30/9/2011.....

SHERIA ZA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MADINI YA UJENZI) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA/UJIJI, 2010

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1 Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji, 2010 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:-

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji;

"Madini ya Ujenzi" maana yake ni kokoto,mchanga, na mawe,

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Sheria" maana yake ni sheria za Fedha za Serikali za Mitaa;

ushuru

4 (1) Halmashauri itatoza ushuru wa madini ya ujenzi kutoka kwa wachimbaji wa madini hayo waliopo katika eneo la Halmashauri kwa viwango vilivyotajwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba au kuhamisha madini ya ujenzi kutoka eneo la Halmashauri bila kibali cha Halmashauri.

(3) Mchimbaji atawajibika kulipa ushuru kwa Halmashauri au wakala aliyeteuliwa kukusanya ushuru huo kwa niaba ya

Halmashauri.

Uwezo wa wakala

5 (1) Halmashauri inaweza kumteua mtu binafsi, kampuni, asasi au Taasisi kukusanya ushuru wa Madini ya ujenzi kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa atakuwa na majukumu ya;-

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri;

(c) kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi;

Makosa kwa wakala

(3) Itakuwa ni kosa kwa wakala yeyote chini ya Sheria Ndogo hizi;

(a) kushindwa kuwasilisha fedha kwa kiwango kilichoainishwa katika mkataba bila sababu za msingi;

(b) kukusanya kiwango zaidi ya kile anachostahili kukusanya

Maeneo yanayoruhusiwa kuchimba madini

6 (1) Halmashauri itatenga na kutangaza maeneo yanayoruhusiwa kuchimba madini ya ujenzi.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba madini maeneo ambayo hayakuruhusiwa na Halmashauri.

(3) Mchimbaji yeyote wa madini ya ujenzi atatakiwa kuzingatia Sheria za hifadhi ya mazingira, na Halmashauri itakua na uwezo wa kusimamisha shughuli za uchimbaji iwapo itathibitika kwamba kufanya hivyo ni muhimu ili kudhibiti uharibifu wa mazingira.

Msamaha wa ushuru

7 Halmashauri inaweza kuruhusu madini ya ujenzi kuchimbwa au kusombwa bila kulipiwa ushuru kwa kibali maalum kitakachotolewa na Mkurugenzi.

Maeneo yaliyopigwa marufuku

8 Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba madini ya ujenzi katika maeneo yafuatayo:-

(a) maeneo ya hifadhi;

(b) maeneo ya mito au kando ya mito na vyanzo vya maji;

(c) maeneo ya karibu na makazi ya watu;

(d) ndani ya mita thelathini kutoka kwenye ukingo wa barabara; na

(e) maeneo mengine ambayo yametajwa katika Sheria yoyote andishi kuwa haifai kwa shughuli ya uchimbaji wa madini ya ujenzi.

Muda na mahali pa kulipia ushuru

9 Ushuru wa Madini ya ujenzi utalipwa wakati gari linapotoka katika eneo yanapochimbwa madini hayo.

Makosa na adhabu

10. Mtu yeyote ikiwa ni mnunuzi, muuzaji au wakala ambaye-

(a) atakataa au kukwepa kulipa ushuru;

(b) atamshawishi mtu yeyote au kundi la watu wasilipe ushuru

(c) atamzuia Afisa Muidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake;

(d) atachimba madini ya ujenzi mahali ambapo hapajaruhusiwa chini ya Sheria Ndogo hizi

(e) atadanganya na kuhusiana na kitendo chake hicho ataikosesha Halmashauri mapato yake;

atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi na atashitakiwa mahakamani akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

JEDWALI LA KWANZA

USHURU WA MADINI YA UJENZI

Na	Aina ya madini	Ushuru (yanayosafirishwa ndani ya nchi)	(yanayosafirishwa nje ya nchi)
1	Mchanga	2,000/= kwa tripu moja	3,000/= kwa tripu moja
2	Mawe	3000/= kwa tripu moja.	7,000/= kwa tripu moja
3	Kokoto	2,000/= kwa tripu moja.	3,000/= kwa tripu moja

Nembo ya Halmashauri imebandikiwa kwenye Sheria ndogo hizi kufuatia Azimio la Kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika tarehe 31 Julai, 2009

Nembo hiyo imebandikwa mbele ya:-

LEWIS. K. KALINJUNA
Mkurugenzi
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI

SHABANI MAMBO
Naibu Mstahiki Meya
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI

NAKUBALI

MHE. MIZENGO. P. PINDA
WAZIRI MKUU

DODOMA..29/7/2014..